
Itakuwa aibu sana watu wa Umande wanatarajia niongee maneno ya maji huku lakini kwa wiki mbili ninaongea hadithi nyingine. Itakuwa aibu sana watu wa Marmanet kule Kinamba wanatarajia tuongee maneno ya kahawa mswada uliokuwa hapa na bado tunaendelea na hadithi nyingine na hawajawahi kusikia hayo maneno ya kahawa. Itakuwa aibu sana wakiona kila siku wakitarajia lile ambalo walinituma na mimi ninatekeleza lile ambalo pengine tunajiambia. Ni vyema nilindwe kwa njia ambayo ni sawasawa ili nipiganie watu wa Umande na mwingine alindwe sawasawa ili awapiganie waliomleta. Isije ya kwamba biashara itakayofaidi watu wa Umande inakandamizwa na mtu mwingine pengine haelewi kile kilimfanya atumwe huku.

Lazima tusimame sawasawa na hili Bunge liheshimike sasa, kesho na kesho kutwa. Kuheshimika kwa Bunge hili ni kufuatwa kwa sheria. Karani wa Bunge hili ama mtu yeyote hata mimi, hakuna mtu ambaye sheria haimguzi. Kila mmoja anaguzwa na sheria kwa maana sheria ni ya Kenya nzima. Kesho tutaongea maneno ya Mugweru na mwingine lakini wote ambao twawaongea kuwahusu tuwe tumelindwa na kuongozwa na sheria ambayo inafaa. Tusije tukaingia mitindo ya kule kwingine ati kwa sababu walirukaruka nasi turukaruke. Ati kwa sababu wengine walilala kwa barabara nasi tufanye hivyo. Sisi ni wasomi na tunajielewa. Tunaijua sheria na tutaifuata leo, kesho hadi mwisho.

Hon. Salma Zamazam: Asante sana Mheshimiwa Spika. Waswahili wanasema ukiona vyaelea ujue vimeundwa. Ninachukua nafasi hii, ninafikiri ningependa kuongea kukiwa na Spika wa Bunge, lakini pia wewe nakuheshimu kwenye kiti chako. Ninasikia kuna kukaangwa tukiwa hai. Vitisho na matusi tumeyapata, tumeshtuliwa kwa mambo mawili matatu hadi mashinani tunatusiwa. Tumeambiwa mambo mengi lakini nimeapa sitabanduka. Hata hayo majina hadi sijui tulifanya nini ndipo tukafika hapa na wanataja watu wa ngazi za juu tumefikishiwa. Unajua hakuna chungu na tamu, hata wao kuzunguka na majina yetu sisi Wajumbe maalum kuwa tuliletwa hapa na watu hadi wanawataja watu hao tutawafikishia na waweze kutuambia vizuri. Kuna Waheshimiwa hapa wanatishiwa na hatuogopi. Tumesikia kwa runinga tulionekana, wacha hata kupiga mayowe, hata kutoa nguo tutatoa.

Mimi kama Zamzam nilitumwa na chama cha Jubilee kikiongozwa na Rais Uhuru Muigai Kenyatta kuwawakilisha walio wachache. Sio wadi moja ila Kaunti nzima ya Laikipia. Nitarudia na mnukuu, sisi kama wafugaji hatujapewa haki na tumenyanyaswa. Nitarudia hilo leo, kesho na hata milele. Hapa sijitetei kibinafsi niajiriwe mtu lakini wacha tufuate ukweli na haki. Tumwachie Mungu wa Yakubu na Yusufu apambane na hao. Ninawahakikishia kabla ya mwisho wa mwezi huu Mungu atakuja kuwalipa hapa. Watu wamesema hawajatumwa kuja kupigana ila kuleta maendeleo. Nimetumwa hapa kuwapigia watu kelele na kuwatetea wengi walio kule mashinani ambao sitawataja majina, wafugaji na walio wachache.

Sijatumwa hapa kujitetea kibinafsi ati ndio niseme nimetumwa na watu wa sehemu fulani kujitetea. Sijakuja hapa kujitetea kibinafsi. Nikiendelea na ninaheshimu Bunge lako vile

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

umeweza kutusomea hadi sheria wiki iliyopita tuliomba mtuletee huo mswada na tunasikia watu walikuwa gangari. Kuteleza sio kuanguka, pia sisi tulijipanga gangari na ndipo tukaja Bungeni. Hakuna vitisho baridi wala moto, hatutaogopa vitisho hivyo. Ninaomba hiyo afisi yako ikiwa hapo kunavyo vitisho vingi sana tumevipata na maneno hayo yako mbali sana. Hatutarudi nyuma kwa sababu ya vitisho baridi. Unapigiwa simu unaambiwa uko hapo kumpiga Spika ati ndipo tumweke Mheshimiwa Matunge. Hakuna siku nitampiga Spika, nitasimama na Spika sio leo wala kesho tu. Hayo tumeyakanusha madai ya uwongo na kueneza madai mabaya ndipo Spika afikirie mambo mengine.

Mimi sitaogopa! Silali kwa mama ama baba ya mtu. Hili ni Bunge la kuongea uhuru. Tukitoka hapa nenda unikejeli, tumeyasikia hayo yote. Ukiwa mtu mkamilifu mpate Mheshimiwa Zamzam, mwambie ndipo ukipate hiki kiti kwa ukamilifu wewe ulienda na mtu fulani. Sitaogopa mbele ya kumbukumbu, wacha kuzunguka na majina yetu bwana! Kuja moja kwa moja kama ni Spika, huu ni mswada wa Bunge sio wa nje. Hata ukiona tumepigania mahitaji ya wafugaji yaangaliwe katika Kaunti ya Laikipia. Kwa hili Bunge ninawakilisha Kaunti nzima, sijatumwa kwa wadi kidogo. Kama utatudharau eti tumeletwa hapa kwa sababu ya nini, hata ukicheka na useme nini Mheshimiwa Zamzam hatabanduka.

Laikipia Kaskazini sasa hivi tuko na mambo ya usalama hatulali usiku na mchana. Bado tuko na mambo ya usalama na tunafinyiliwa mambo ya uajiri. Vijana wetu mnataka waende wakuwe wezi? Sijakuja kujitetea kibinafsi, hakuna mfugaji amenung'unika vile nilikuwa ninafanya. Sijui kama kulikuwa na manung'uniko ukiwa kwenye hicho kiti na niko na haki ya kuongea. Ukiongea ukitutishia na kuzunguka ati Mheshimiwa Zamzam alikuwa na nani hayo ni yako na hayatutishi. Wacha nikwambie kama unanitaka njoo moja kwa moja, wacha kuwasumbua watu huko. Ala! Kwani namna gani? Unajua sisi Wasomali huwa tunasema kila nafsi itaonja mauti na ni siku moja na dakika.

Kwa hivyo Bwana Spika sisi tunaomba utuheshimu hata kama hatuna namba. Ulete mswada wetu kwa sababu hakuna mtu tumekuja kupiga ili tuendelee na Bunge. Hili Bunge ni la heshima na hatubebani ugomvi mpaka kwa mitandao au matusi kubwa na hatungetaka ifike hapo kwa sababu sisi wote ni marafiki. Ikifikia upande wa kukwaruzana itategemea kwa urefu wa meno na ukali wa kucha.

Hakuna mtu ambaye alikuja hapa kusumbuana ama kuonekana chama kilichomleta. Wakati mwingine utaniona kwa cheo fulani hadi ushtuke. Wewe sio Mungu, kwa hivyo wacha kukejeli watu na kuwasurubu. Ya Ndai na Biwott ililetwa kwa hili Bunge na hakuna mtu ambaye alidharau. Kila mtu alikuwa kipao mbele ya kuleta hizo miswada za kuwaondoa. Kulikuwa na zingine ambazo zilikuwa zifuate lakini hatukuwa na huo ugomvi bali tulielewana. Sijui ni nini hiki kinafichwa hadi watu wanakuwa *personal* hadi unatumiwa watu. Wacha hayo mambo bwana. Chunga usininyooshe kidole cha lawama nami nikunyoshee tano.

Kila mtu hapa yuko na akili yake na tunajua kila kitu. Kwa hivyo kama ni kuelewana vile Kanyutu na Mutahi wamesema, tuketi chini maana hakuna MCA mkuu. Mimi ndiye MCA mkuu ambaye anapigania wafugaji Kanti la Laikipia. Mheshimiwa Spika, wewe ukiketi kwa hicho kiti mimi nakupigania wewe mwenyewe na hata Jacob Endom. Mimi napigania wafugaji wangu na sitarudi nyuma kwa sababu sikuletwa hapa kuwa maua ya kaunti.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Deputy Speaker: Order Hon. Hussein! Sorry for that interruption. Hon. Stephen, any other time stop echoing any other Member. You may proceed.

Hon. Salma Zamzam: Bwana Spika, nimesema hata wewe ukiketi hapo ninakupigania na ninapigania haki yetu kwa sababu sikuletwa kuwa maua ya Kaunti eti watu wanashangaa tukibishana. Tumbo yenye imeshiba haijui yenye imelela njaa. Mimi narudia kusema ya kwamba watu wangu walifurahi sana mpaka Kaunti zingine za jirani kwa sababu tulikuwa tumenyanyaswa. Kila mtu anaongelea watu wake kama vile Mheshimiwa ameweza kuongea kuhusu watu wake wa Umande. Kwa kweli tukiangaliwa hivi na wafanyikazi wa hii Kaunti unaweza kuta ya kwamba wafugaji ni 5% pekee na wako kwa cheo kidogo sana. Ndio maana mimi nalilia haki.

Hata ukinicheka, unikejeli ama uniangalie vibaya mimi nitaongea usiku na mchana na nitatea hao wafugaji ambao walionileta kwa hili Bunge. Uhuru Muigai Kenyatta akiwa pale pia ananiangalia kwa sababu alinituma hapa kwa sababu aliona inafaa Zamzam anafaa kutetea wafugaji. Ni kwa nini nimuangushe chini au niangushe wachungaji. Sisi tulikuwa tunaomba hata kama ni kupandishwa cheo waangaliwe na tusitoke nje kama mswada haujafika kwa sababu ombi letu ni huo mswada ufike.

Tumesikia ya kwamba HBC ilifanya kazi ya busara na ni sawa. Uongozi wa hili Bunge haujajumuisha wanawake. Mimi ningekuwa pale ningesukuma hao wanaume waone kama mambo inaweza kuwa sawa. Hamuoni kina mama ambao muko nao ndani ya nyumba ambao ni bibi zenu na mama zenu? Kwani hamtumii sheria ya kijinsia? Hata hayo maneno tutaangalia. Mimi sina mengi bwana Spika. Asante kwa kunipatia huu muda hata mtu akisimama anikosoe nilikuwa ili shida yangu iangaliwe.

Hata hao wafugaji waangaliwe zile cheo ambazo wamepata turudi tuangalie kama wako na shahada na kama wanaweza pata cheo kubwa kama ya HR. Ninaheshimu hili Bunge na nitazidi kuiheshimu na hata leo ikitakikana twende tuone kama iko na sarakasi ni sawa tu. Kama kutetea haki imekuwa aibu, mimi sio aibu na hata kutoa nguo inawezekana. Mtu asiabike kwa sababu nimeongea kwa sababu nililetwa na chama nitetee watu wangu wafugaji ambao masomo na barabara zimekuwa shida. Kila siku tunasumbuliwa na hata tunasumbuliwa kwa ajira. Ninasema kwa sababu ya akili yangu na kama imekuuma naomba unisamehe. Tukitoka nje usiniangalie vile tunavyoangaliana hapa karibu uteme mate. Wewe nisalimie kwa sababu naenda kulala kwangu.

Hon. Jacob Endom: Asante sana, Bwana Spika. Nafikiri yangu ni chache kwa sababu ni tu kuambia Waheshimiwa ya kwamba hili Bunge ni letu zote. Siasa za Bunge hazijaanza leo lakini zilianza kitambo na hata tulipata zikiendelea. Wengine hapa mukiona siasa za Bunge mnaanza kukasirika na hamna urafiki na mtu. Sisi wengine tulizoea siasa. Hata Mheshimiwa Robert leo nimekupigia simu kwa sababu ninajua ya kwamba siasa itaishia hapa na tukitoka hapo nje tuendeleze maisha kama kawaida. Wengine wanaona eti tukilimana hapa ni kama hata hapo nje hatuwezi kunywa chai.

(Deputy Speaker left the Chair)

(Speaker took the Chair)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mimi nililetwa hapa na watu wa Sosian na sio kwa uzuri. Nililetwa kama mwenda wazimu ili niache wengine wazuri huko. Kwa hivyo ndio maana mnasema ya kwamba Jacob ni MCA mkuu. Niliambiwa niache wengine huko mashinani ili nami nije niwakoroge hapa. Kwa hivyo ile kitu ambacho mnafanya mimi sioni kama mnafanya vibaya kuleta mjadala lakini tufuate ile njia ambayo tulifuata wakati ambao tulileta mjadala wa Ndai. Tuliitana na tukakaa pamoja na tukasema tutaelekea hivi lakini sasa nyinyi ndio mulienda vibaya wakati mlienda kugawanya. Mkaenda katimu fulani ikaenda kuanza vita na timu nyingine. Kama mwanaume ukiona vita ikija ni lazima upigane hiyo vita. Ndio mimi ninawaambia ya kwamba walete huo mjadala kwa sababu tuko tayari kama hiyo ndio inaleta vita kwenu.

Juzi tulikutana kwa hili Bunge na hata hatukuwa tunajuana na hili Bunge ndilo limefanya tujuane. Sisi wengine ni watu wazima ambao hatulingani kwa miaka kwa sababu wengine kama sisi ni wazee na hatuwezi kubali ile sarakasi ambayo mnaendesha hapo nje. Mzee kama mimi ambaye niko na watoto zaidi ya thelethini nikionekana nikifanya hiyo tabia hapo watoto wangu watauliza ni tabia ipi hiyo. Ndio maana mimi niliondokea nikasema hawa vijana waende wafanye sarakasi yao huko. Mtu kama Kaparo akionekana huko ni aibu. Kwa hivyo mimi nikiona Chris Mark akifanya, yeye ni kama *my daughter* na akifanya vile hiyo ni kazi yake. Akifanya hiyo kazi mimi kama Jacob ninafurahia.

Hon. Simon Kanyutu: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa wa Sosian amesema ya kwamba Chris Mark ni msichana wake. Mheshimiwa Jacob anachanganya lugha na ndio maana amesema ya kwamba Mheshimiwa ni *Daughter*. Labda anaweza kutuelezea ni kwa nini anaita Mheshimiwa Chris Mark msichana wake.

Hon. Jacob Endom: Asante sana, Bwana Spika. Ndio maana niliambia Waheshimiwa tukubaliane na tucheze kwa sababu hii biashara tutaifanya vile tulikuwa tumefanya hapo awali kwa sababu sisi hatukuwa tumekataa hii kitu. Tufuate utaratibu tulioufuate na tuendelee. Mlivyofanya sio vibaya kwa sababu ni lazima muamshe watu akili ili wajue ya kwamba nyinyi ni viongozi wa hili Bunge lakini sio vita na kujibizana na kupigana kifua.

Mimi nimetoka Sosian na kulingana na yale maisha ambayo iko huko ni ya wafugaji. Sisi hulimana huko lakini wazee wakiingia kati kati hayo maneno yanaisha. Kwa hivyo mimi naambia Waheshimiwa ya kwamba ni vizuri kuitisha kikao tukae kwanza ili tuongee kama wazee wa nyumba. Mukiongea mshindikane, basi tutaleta kila kitu kwa sababu vita iko kila mahali hata kwa serikali kuu na hata manyumbani. Wanafanya sarakasi hapo nje hadi watoto wanalia. Kwa hivyo mimi sioni kama ambayo mnayoifanya hapa ni mbaya. Hayo ni mambo ambayo hii dunia yote inaelewa. Ningetaka kusema ya kwamba tuheshimiane kwa sababu hatulingani na tuko na mila tofauti. Kitu kizuri ni tuwe kama viongozi ambao walichaguliwa na wananchi ili tuwatetee.

Tuliletwa hapa na wananchi ili tuwatetee na tuone ya kwamba wamesaidika. Tusione ya kwamba ni kama kwa hii miaka mbili ambayo imebaki ni kama wananchi hawaoni ni nini ambacho tunafanya katika hili Bunge. Kuanzisha heshima yako hapa itafika hadi huko kwako na watajua vile uko kwa sababu hatukuchaguliwa kimakosa. Walituchagua wakijua ya kwamba sisi ni viongozi wao ili tuwatetee tukiwa tumechaguliwa au kuteuliwa.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kwa hivyo naomba mutulie na Bwana Spika uitishe kikao kwanza ili hawa watu wakae chini watoe maoni yao. Niliona hata kwa Bunge la Taifa watu 180 wakitia sahihi lakini wakati walienda kikao wakamaliza kwa hicho kikao chao. Kama hawaridhiki basi mjadala ije katika hili Bunge kwa sababu ikija hapa wanaume watanyoroshana na huwa maridadi kwa sababu tukinyoroshana hapa hakuna hata siku tena mimi nitaleta mjadala wangu uniunge. Utakuwa unaunga biashara ya kwako na ile timu ingine ambayo itashinda iunge timu yao na hiyo ni kugawa Bunge na kama kiongozi singetaka hivyo.

Kwanza nilikuwa nataka mshikane muongee kama watu kwa sababu sisi ni kama mandugu tukiwa hapa na kwa hivyo ni vizuri sana kwanza kujadili. Wacheni kujionyesha ya kwamba nyinyi ni wenye nguvu. Miaka mbili iliyobaki hiyo nguvu yenu itakuwa imeishia kwa wananchi. Huku mnapigana na kwa wananchi mnanyoroshwa. Tengeneza wananchi kutoka mashinani na ukija hapa uwe ukijua ya kwamba ukirudi pale wananchi watakuchagua tena lakini kuna kazi bure hapa kwa Bunge haitawasaidia.

Bwana Spika, mimi kama Mheshimiwa wa Sosian leo hii ninaomba kitu moja. Nimesikia Mheshimiwa Mutahi na Kanyutu akitaja hilo jambo la kuitisha kikao ili tuwasikize na kama hawatakubaliana basi wacha itandikwe kwa meza na tuumane kwa hiyo meza. Leo kila mtu alikuwa anajua atakuja kuongea nini hapa kuhusu huo mjadala. Msijipige kifua kwa sababu hata Ndai tulimsukuma na nyinyi mbali na sasa yuko kwa ofisi. Hiyo ikija hakuna mtu ambaye alikuwa anapinga kwa sababu mimi niliwaita na tukakaa chini zote na kukubaliana kwa sababu makubaliano ni mazuri sana katika hili Bunge.

Hakuna mjadala mwingine wowote ambao uliwahi kuleta tata kama huu katika hili Bunge. Umeleta tata kwa sababu hatukukubaliana kwa kikao. Tungekubaliana huu mjadala ungekuwa umepita kwa ule utaratibu ambao unastahili. Kwa hivyo Bwana Spika mimi nitafikisha hapo na ninaambia Waheshimiwa wacheni kupigana kifua na kujifanya ya kwamba nyinyi ni *Dictator*. Kwenda ujifanye *Dictator* kwa ile wadi ambayo wewe umechaguliwa kama vile mimi ni *Dictator* wa Sosian lakini sio hili Bunge. Mmesikia? Wewe kama unawakilisha kwako kwa kupiga kifua, mimi hautanipigia kifua kwa sababu hautanitoa. Nililetwa hapa na watu wa Sosian na hao ndio watakaonitoa ikifika wakati wa kutolewa wakiniambia ya kwamba sikufanya kazi nzuri na wanielekeze nyumbani lakini sio nyinyi.

Juzi niliwaambia ya kwamba siwaogopi na tutalimana na nyinyi hadi dakika ya mwisho. Kwani nilichaguliwa kwa uzuri ili nije hapa? Si walijua ya kwamba mimi ni mkorogaji wa watu huko kijijini na ndio wakanileta hapa. Mheshimiwa rafiki yangu huko mwenyekiti wangu wa CPAIC, mimi tu ni kama wewe. Ukichemka ninachemka na ukitulia pia ninatulia. Si unaona ya kwamba nimetulia? Kwa hivyo tutulie vile Mheshimiwa Mutahi alisema wacha twende tukae kama wazee tujadiliane na tutoe maoni yetu. Nilipenda vile Mheshimiwa Mutahi na Kanyutu walisema ili tumalize hiki kitu kwa kikao.

Bwana Spika, sisi tulikuwa na desturi ya kwamba ni Waheshimiwa pekee yao ambao tulikuwa tunakutana halafu tunanyoroshana. Hatutaki mtu mwingine ndani na mtu aache kusema ya kwamba ameteuliwa kwa sababu ukiwa kwa hili Bunge wewe ni Mheshimiwa. Ule mshahara ambao mimi hupata ni kama ule ule tu mimi napata. Kwa hivyo tuweke heshima na tuwache vita. Kwa hivyo nafikisha hapo na ninashukuru kwa hiyo nafasi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Salma Zamzam: Asante, Bwana Spika. Ningetaka kuarifu ndugu yangu na ni asante kwa sababu ametuambia ya kwamba sisi Waheshimiwa sote ni sawa na sio kwa mshahara pekee. Mimi nawakilisha Kaunti nzima ya Laikipia kuanzia Mukogodo ya chini mpaka wa Isiolo, Turkana hadi Baringo. Mimi huwa na kazi kubwa sana ni vile nyinyi huwa hamjui. Ninashindwa hata kufika huko kwa sababu ya *mileage* wakati mwingine. Kwa hivyo mimi huwakilisha watu wengi hata kumshinda yeye.

Hon. Jacob Endom: Bwana Spika, ninashidwa ni kwa nini Mheshimiwa anaongea hivyo. Unajua mtu huanzia hivyo tu akitaka vita na mtu na mimi sina vita naye. Wacha tu ninyamaze.

Speaker: Nilikuwa nataka Mzee Kaparo atufungie lakini wacha nipatie Mheshimiwa Kaparo halafu Naibu wa Spika atufungie.

Hon. Chalumbo Ole Kaparo: Asante sana, Bwana Spika. Ninashukuru Mwenyezi Mungu na kila mmoja wetu na pia wale ambao wamechangia tangu saa nane na nusu. Nimeketi hapa na kuangalia na nikasikia na hata nikaona. Nimeona yale mambo ambayo inaendelea hapa lakini nikiangalia sijaona jambo lolote ambalo limeendelea vibaya kwa sababu kila Mheshimiwa hapa ameongea yake. Kila Mheshimiwa ambaye amesimama hapa aliletwa hapa kwa njia yake na ameongea kwa ile njia ambayo inamfaa.

Mheshimiwa Spika, tangu sisi tuje kwa hili Bunge hasa mimi ambaye nimekuwa kwa hili Bunge tangu 2013, wengine walinikuta na wengine tumekuwa pamoja. Mimi sina akili zaidi kuliko wale ambao walikuwa hapo awali ama wale ambao walinikuta hapa. Hata yule ambaye alikuja jana ako na akili kama mimi au hata zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri watu kuongea mchana kwa sababu sisi jamii zingine husema ya kwamba tukiongea mchana tunaangalia kwa macho na tukiongea usiku tunasikiza roho. Sio vyema Mheshimiwa yeyote akisimama hapa na wengine wanacheka huko na kuongea chini chini. Haina maana, sikiza yeye na wewe pia upate nafasi yako ya kuongea yako. Mimi kama mwakilishi wa watu wa Segera hasa nimewakilisha Segera mara mbili na sijakuwa nikiwakilisha kwa nusu akili lakini akili yangu ikiwa sawa. Ninasimama hapa na hakuna siku yoyote ambayo nitasukumwa na mtu niseme yale ambayo sikuwa nataka kusema. Hakuna siku ambayo pia nitakayounga mkono mtu yeyote au kundi bila akili yangu kunielekeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa yeyote ambaye ameongea kutoka saa nane na nusu ninawapongeza kwa sababu hiyo ndiyo kazi yao ambayo imetuleta hapa. Kazi ya Bunge la kitaifa na la Kaunti, kwa watu ambao wanaelewa mambo ya Bunge, sio maneno ya kupigana lakini ni ya kuongea na watu kucheka. Kwa mfano sisi tulikuwa kwa hili Bunge tukiwa na mjadala wa Katibu wa Kaunti. Mimi nilikuwa kwa upande wa kuunga mkono na tukaangushwa katika hili Bunge lakini sikukasirikia mtu yeyote. Tulitoka hapa tukiwa marafiki tukijiambia ya kwamba leo tumeshindwa lakini kesho tutashinda na hiyo ndiyo kazi ya Bunge ambayo nataka tufanye.

Mambo ya kuita wengine majina haistahili lakini inastahili tupeane heshima kwa sababu Waheshimiwa ni watu ambao wameheshimika na wale watu ambao wako nje. Yeye mwenyewe hajiiti Mheshimiwa lakini wale ambao wamemleta hapa ndio ambao wanamuita

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mheshimiwa na wanajua ya kwamba yeye ni Mheshimiwa. Bwana Spika, kidogo nimekereka roho kwa yale ambayo yanaitwa porojo. Wengine wanasema ya kwamba wale Waheshimiwa wa zamani ndio ambao wanatumika vibaya kwa hili Bunge.

Wengine wanasema ya kwamba mtu kama Kaparo ambaye ametoka kwa upande ulio na wachache. Ndio nimetoka kwa wachache lakini ningetaka niulize ambaye alikuwa ameleta porojo, je wale wakikuyu ambao wako Segera, hawana haki ya kupata kazi? Hao wakikuyu wanaangalia nani kama mwakilishi wao? Hiyo ndio porojo ambayo ninasikia na ninasema ya kwamba wale Wakikuyu ambao wako Segera ninawahesabu kama wachache na huo ndio ukweli wa mambo na nitasimama na hayo na nitazikwa nayo.

Mheshimiwa Spika, ule mjadala ambao kila mmoja wetu alikuwa anatarajia ifike hapa, mimi niko katika HBC lakini Waheshimiwa walisomewa sheria na mimi naona ya kwamba kuna mahali umetusomea vizuri. Ninaamini ya kwamba huo ndio ukweli. Nikisimama hapa na nitake kutoka nje sitapita kwa ukuta lakini nitapita kwa mlango kwa sababu hakuna mtu ambaye amekataa mjadala. Mimi kama nitapiga kifua niseme ya kwamba huo mjadala uje tuangushe au tupitishe, haistahili. Wewe tafuta namba na utafute kwa njia iliyo halali. Tembea usiku kama vile unavyosema ya kwamba mikutano ilifanywa. Hiyo ni porojo tu. Ni nani ambaye amekukataza ufanye mikutano yako?

Hiyo haistahili hapa. Wewe enda ufanye mkutano na uende usiku kama vile umesema ya kwamba wengine wanafanya. Hata mchana nitafanya jua ikisimama lakini ile ya muhimu zaidi ni heshima kwa hili Bunge. Kutofautiana katika hili Bunge sio kitu geni au ya kukasirisha watu na kutengana lakini hiyo ni kawaida ya siasa. Wale wengine ambao wanajua kidogo mambo ya siasa ambao ni wa zamani walioitwa Madiwani, wakati wa kuchaguliwa diwani mwenyekiti wengine walikuwa wanapelekwa Nairobi na unasikia mwingine ashachaguliwa. Wengine walikuwa wanapelekwa Mombasa kuvishwa na sio vita bali ni mbinu ya kutafuta.

Kwa hivyo Waheshimiwa hata tukiendelea kuongea kuhusu huu mjadala sisi ni watu ambao wameheshimiwa na tunawakilisha zaidi ya watu elfu mia tano katika Laikipia. Hakuna Bunge la pili bali ni hili tu ambalo watu wa Laikipia wanaangalia. Wanajua ya kwamba wamewatuma hapa ili muwaakilishe. Watu ishirini na nne wanawakilisha watu elfu mia tano. Fanya hilo hesabu, mtu mmoja anafaa kuwa anawakilisha watu wangapi?

Kwa hivyo Waheshimiwa watu wanatuangalia usiku na mchana. Mimi nimalizie nikisema ya kwamba mambo ya kuongea huko nje na kupigana ni tofauti na hili Bunge. Wale ambao wanaelewa kwa sababu kuna wengi ambao wanaelewa mambo ya Bunge ya Kitaifa, sisi tunaelewa kidogo na kwa hivyo hatuwezi kuongea maneno ya mtu ambaye amefungwa mdomo hapa kama mfanyikazi na pia hana nafasi ya kuongea hapa na pia hajawahi kusikika mahali. Kwa hivyo Waheshimiwa twende kwa utaratibu na kama ni mjadala hapana jipiga kifua sana. Itisha tu kwa utaratibu kwa sababu unaweza kujipiga kifua na huo mjadala wako uangushe na wewe utaendelea. Kama huo mjadala ulikuwa umeletwa hapa ungekuwa umeangushwa kitambo ama ukapita. Sisi basi tungekuwa na biashara ingine.

Waheshimiwa, isiwe ni biashara ya kuja kutugawa hapa. Kama mtu ana makosa yoyote na hakuna utaratibu wa kumtoa hapa, basi ni wewe na mimi. Hakuna yeyote hapa ambaye anaweza kuleta mjadala wa kutoa Kaparo au Mheshimiwa yeyote hapa. Ule mjadala ambao

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

unaweza ukaletwa hapa labda watu wa Segera waje na hiyo siku kwanza ninaweza kupitishwa mlango wa nyuma.

Mheshimiwa Spika, mimi narudia vile wengine wameomba ya kwamba usimame imara na usimame katikati kwa sababu hawa watu wote ni wako wenye wameleta mswada na pia wenye wanapinga. Hakuna haja hata siku moja uwe ukipendelea mtu yeyote hata kama ni mimi Kaparo. Simama katikati kwa hicho kiti ambacho tulikupatia mchana bila kupendelea yeyote. Kama Kaparo analeta mjadala ambao hauko kwa sheria basi simama kwa sheria na hilo ndilo kauli langu.

Ninaomba tuheshimiane na tuepuke maneno ya kutusiana katika hili Bunge hata kama maoni yetu ni tofauti. Vile *Serjeant at Arms* wameletwa hapa kujaza Bunge sio makosa kwa sababu wanalipwa na serikali na wako na haki ya kukaa popote na kwa hivyo sioni wakiwa na makosa. Waheshimiwa kama ni mimi naulizwa ninaweza sema tuheshimu kila mtu hata kama anatoa maoni tofauti na ya mwingine. Mimi nimekuwa nimeketi tangu saa nane na nusu na sijashangilia mtu yeyote au kuongea kichini chini kwa sababu ninaheshimu kila mtu. Nitaendelea kusimama na watu ambao wanajiita wachache. Asante.

Hon. Daniel Nyausi: Thank you, Mr. Speaker for giving me this chance to comment on the communication that you have made. Allow me to start by saying that that motion tried to find its way last week but it did not make it to HBC. I need to thank you because I told you that there is a need for us to have an extra HBC meeting on top of the one that we usually do per week and you agreed but unfortunately the HBC Committee did not have a quorum. We could not also proceed without quorum because it is the law.

Mr. Speaker, today when we received the same motion, I used the wisdom of the same committee that that motion cannot find its way in this House. We are here serving this House as well as protecting it and we will not go in a way that will demean the standards of this House. We must always protect and uphold this House by ensuring that this is a House of order and respect.

Mr. Speaker, that is not the end because there is a process to go about that. We are very happy that there is still a way so that at least the Members can quench their thirst. I might not be seeing that thing today but it can help me. So it is always good to listen and I will urge the Hon. Members to follow the rules and procedures to make sure that we will get what we think is good for our people.

Mr. Speaker, also allow me to say that we have got a few Members commenting on why we have the Serjeant at Arms guarding the Mace and why the doors are closed. If tomorrow it will be raining nobody would ask me not to take an umbrella or a heavy coat because of the weather. All of us have got different duties and therefore if the Serjeant at Arms sees that the weather is not good for their job, they have to do what they think is right for them including closing the doors because that is their work.

So let us respect each other and follow the right procedures. At least I am happy that we have got a communication. Members, please let us learn not to force for illegality but always try to find new means for our voices to be heard in the right way. Thank you.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Catherine Kibue: Asante, Mheshimiwa Spika. Kwanza nikushukuru kwa mwongozo ambao umetupatia. Ningetaka kusema ya kwamba wakati hauko na kwa sababu ofisi haijafungwa, ningefurahia kama tungeongozwa vile umetuongoza kwa sababu kama tungekuwa tumepewa haya maagizo wiki iliyopita, hatungekuwa tumefika hapa.

Hon. Daniel Nyausi: I need a bit of clarification Mr. Speaker. I would like the Member to clarify to this House, how could the communication be given out if the matter had not been heard. Mr. Speaker, the committee that is supposed to approve the business of this House did not meet to approve this matter. So then how do you expect the communication even before going the said motion?

Hon. Catherine Kibue: Asante sana, Bwana Spika. Ningetaka kufahamisha ndugu yangu ya kwamba tulienda kwa ofisi ya naibu wa karani na akatupa maagizo na akatusomea sheria na tukafuata. Kwa hayo Bwana Spika, sitaki kusema mengi kwa sababu wengi wamesema. Ningetaka tu kusema ya kwamba *'mgala muue na haki umpe'*. Kwa hao wanyonge kwa hili Bunge tungeomba ya kwamba tupewe haki yetu. Mimi kama Catherine ninasimama kwa miguu yangu na ninasema ya kwamba hao ambao wanaenda kwa hizo mikutano wanabebewa akili. Mimi ni mama wa watoto wawili na ni bibi ya mtu na kwa hivyo sibebewi akili na mtu na ninasema ambayo iko na akili yangu na pia nafuata dhamiri yangu. Asante.

CONSIDERED RULING

OBSERVATION OF LAW AND ORDER

Speaker: Thank you, So much Hon. Members. We have really deliberated a lot and I would wish to clarify that even when I am not present, my office still works. It is only that this advice could have been given earlier only that HBC Committee did not meet and also the moment when the motion came to the HBC, there was no quorum. Therefore, the other meeting that we have had since that time is today morning and I think that we have advised accordingly.

Hon. Members, I will continue to say that let us be followers of the law and ensure that as we make laws we are also charged to follow the same. We will appreciate as some of us have said that we have heard some impeachment motions in this House of some people who were approved in this House and when that procedure gives us the mandate to do that, then we shall do exactly that.

I believe that there is a procedure to be followed for the removal of the greatest or the smallest man in the land. Let us make sure that we follow that procedure and we guard the laws that we do make. Otherwise I thank all of you for the many remarks and comments that you have made. Mine is to continue asking ourselves to give the Hon. Members of this House and also workers as brothers and each one of us have their different ways of viewing things. When your opinion and mine do not agree we have to respect each other's opinion.

Hon. Kaparo said a very important thing that when we have one Member contributing, let us not make noise but listen to him/her because they are entitled to their opinion. Therefore, it is important for us to respect one another. I know that we as Hon. Members will do exactly that. Before we go to the next order I would still want us to remind ourselves that we are in times of COVID and the COVID rules must be keenly observed so that we ensure that we still

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

do the social distancing here in the Assembly and also outside. Whether we have these issues that we want to express no matter in what manner we must observe the rules.

I believe that we are supposed to protect ourselves because by so doing you protect the other person. It is important so that we do not remain to be asked many questions that we have seen Members in the television and the only issue I had was not for the Members to be seen on television but the issue of having the masks and observing social distance. I have a problem with that and therefore let us ensure that wherever we go as leaders we observe the Ministry of Health guidelines. Even the President of this nation is very clear that it doesn't matter who we are either a leader, a great government official or state officer, let us ensure that we observe the guidelines of the Ministry of Health. I believe that we are going to do that and I hope that we shall adhere to that.

Secondly, as we said we will still have the need to go through the test. It is important as a Member if you can even take the test voluntarily because I have seen a member who went and did the test. Therefore, it is important for us to know our status because when I know my status and if I turn to be positive then I will quarantine myself and I will not risk the lives of others by spreading that disease unknowingly. So it is important for us to know so that you can guard your family and your colleagues and can be able to go and seek medication as required. Therefore, let us make sure that we also voluntarily go and seek to know our status as far as covid-19 is concerned. Thank you, Hon. Members.

MOTION

RECONSTITUTION OF COMMITTEE ON APPOINTMENTS

Hon. Mutahi Muritu: Thank you, Mr. Speaker, Sir. I beg to move the following motion;

THAT, pursuant to the provisions of Standing Order No. 184 (1) and 184(2), this House approves the appointment of the following Members to the committee on appointments;

1. Hon. Patrick Waigwa - Speaker
2. Hon. Peter Thomi - Leader of the Majority
3. Hon. Jacob Endom - Leader of the Minority Party.
4. Hon. Judy Lukio
5. Hon. Joseph Suge.
6. Hon. Patricia Muthoni.

Thank you, Mr. Speaker and I call upon Hon. Matunge to second the motion.

Hon. Peter Matunge: Mr. Speaker, I don't know who advised the Hon. Member to call me to second this motion because I am not ready for any business and therefore I am not seconding this motion.

Speaker: Hon. Mutahi, you can look for another person who can second that motion.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Mutahi Muritu: I call upon Hon. Ndiritu to second the motion.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bwana Spika. Nafikiria ya kwamba kulingana na vile biashara iko na kulingana na vile tunaona katika hii *Orodha ya Biashara*, siwezi kuunga huu mswada. Tunajua ya kwamba sheria inasema ya kwamba wakati mswada umepingwa unakufa hapo na kwa hivyo hatuwezi kubali kitu kama hicho kiendelee hapa.

Speaker: Thank you, Hon. Members. I will give the ruling on that tomorrow on the issue of that Committee on Appointment. There are three Members who are supposed to be approved who are Hon. Judy Lukio, Hon. Joseph Suge and Hon. Patricia Muthoni but I will give a ruling on that. I also know that for that motion where it fails to come to the House again, it will take us another six months. Yes, we have serious business to do on vetting but the only way for it to come is by changing the content of the motion by changing the Members which also will disrupt our committees but since we cannot hold this House at ransom and it cannot even vet the CECM's, I think the better way is to change the names. I think that we can now get into the business of committees.

ADJOURNMENT

Speaker: This House now stands adjourned until tomorrow Wednesday, 18th November, 2020 at 9.00 a.m.

The House rose at 5:20 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*